# DUNIA NZITO INANIELEMEA

*Jackson Kauru*




2.Yesu njoo njoo uniokoe (Bwana)
Dunia ni nzito Bwana inanielemea
Gonjwa zito kama simba mla watu (Bwana)
Linatumaliza Bwana njoo liondoe (Bwana)
Ukimwi ukimwi Bwana unatumaliza (Bwana)
Hauna mkubwa mdogo unapukutisha (Bwana)
Haujali cheo umri Yesu tuokoe.

3.Yesu njoo njoo uniokoe (Bwana)
Dunia ni nzito Bwana inanielemea
Vita chuki wivu vilema vya Roho (Bwana)
Ni mambo mazito Bwana yananielemea (Bwana)
Mimi ni mdhambi Bwana njoo nitakase (Bwana)
Kama ni uzinzi Bwana niache kabisa (Bwana)
Nina majivuno Bwana dhambi ya asili (Bwana)
Kama ni kiburi Bwana shuka kiondoe.

4.Yesu njoo njoo uniokoe (Bwana)
Dunia ni nzito Bwana inanielemea
Mimi mtoto tumboni mwa mama yangu (Bwana)
Nauliwa bure mimi ninaangamia (Bwana)
Mama Baba wote leo wananiondosha (Bwana)
Natolewa mimi bado nikingali mimba (Bwana)
Nimekosa nini Bwana ninaangamia (Bwana)
Wasamehe kwani hawajui watendalo

5.Yesu njoo njoo uniokoe (Bwana)
Dunia ni nzito Bwana inanielemea
Radi mvua jua linaniwakia (Bwana)
Kiumbe mnyonge Bwana ninaangamia (Bwana)
Mimi masikini Bwana nitakwenda wapi (Bwana)
Mimi ni yatima Bwana sina pakulala (Bwana)
Mimi ni mjane Bwana sina msaada (Bwana)
Tegemeo langu kwako Yesu niokoe

6.Yesu njoo njoo uniokoe (Bwana)
Dunia ni nzito Bwana inanielemea
Pombe Bangi na madawa ya kulevya (Bwana)
Ni mambo mazito Bwana yananielemea (Bwana)
Tamaa za mwili Bwana zinaficha Roho (Bwana)
Mshahara wake ninajua ni mauti (Bwana)
Shetani muovu Bwana kaniteka Roho (Bwana)
Kwa jina la Yesu namuamuru ashindwe.